



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



KUMB: PPR/2023 - 02/01

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 1 FEBRUARI 2023

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 1 Februari 2023**. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Kwa Februari 2023, bei za rejareja za mafuta ya dizeli na mafuta ya taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimeshuka kwa shilingi 190/Lita na shilingi 142/Lita, mtawalia, ikilinganishwa na toleo la tarehe 4 Januari 2023 wakati bei ya rejareja ya mafuta ya petroli haibadiliki.
- (b) **Kwa Mikoa ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara)**, bei za rejareja za Februari 2023 kwa mafuta ya petroli na dizeli zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la tarehe 4 Januari 2023. Hii ni kwa sababu, kwa mwezi Januari 2023 hakuna shehena ya Mafuta iliyopokelewa kupitia bandari ya Tanga. *Kutokana na kuisha kwa mafuta ya taa kwenye matanki ya kuhifadhia yaliyopo Tanga, waendeshaji wa vituo vya mafuta kwenye mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kuchukua mafuta ya taa kutoka katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea mafuta ya taa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.*
- (c) **Kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma)**, bei za rejareja za Februari 2023 kwa mafuta ya petroli na dizeli zimeshuka kwa shilingi 118/Lita na shilingi 160/Lita, mtawalia, ikilinganishwa na toleo la tarehe 4 Januari 2023. Kwa kuwa hakuna matanki ya kuhifadhia mafuta ya taa katika bandari ya Mtwara, *waendeshaji wa vituo vya mafuta kwenye mikoa ya Kusini wanashauriwa kuchukua mafuta ya taa kutoka katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea mafuta ya taa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.*

Bei za miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwani katika **Jedwali Na. 1**. Tofauti ya bei kutoka sehemu moja kwenda nyingine inatokana na tofauti ya bandari mafuta yanapochukuliwa na gharama ya usafirishaji.

Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia, gharama za usafirishaji (*BPS Premium*) na thamani ya shilingi ukilinganisha na dola ya kimarekani.

Katika kutekeleza bei hizi, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuzingatia yafuatayo: -

- (a) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (b) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuvi ya bidhaa za mafuta.
- (c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo (Price cap)** au **kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price)** kama ilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 57 la tarehe 28 Januari 2022.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakioneshi bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeliza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (e) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuvi

wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuvi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

- (f) **Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 1. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**
- (g) **Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 2 isipokuwa kwa wateja wenye msamaha wa kodi. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	2,819	3,105	3,061
Arusha	3,036	3,397	3,145
Arumeru (Usa River)	3,036	3,397	3,145
Karatu	3,054	3,415	3,164
Longido	3,047	3,408	3,156
Monduli	3,041	3,402	3,151
Monduli-Makuyuni	3,046	3,407	3,156
Ngorongoro (Loliondo)	3,121	3,482	3,237
Coast (Kibaha)	2,824	3,109	3,066
Bagamoyo	2,830	3,116	3,072
Bagamoyo (Miono)	2,861	3,145	3,102
Bagamoyo (Mbewewe)	2,842	3,126	3,083
Chalinze Junction	2,833	3,119	3,075
Chalinze Township (Msata)	2,838	3,123	3,080
Kibiti	2,840	3,125	3,082
Kisarawe	2,826	3,112	3,068
Mkuranga	2,829	3,114	3,071

JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Rufiji	2,847	3,132	3,089
Dodoma	2,878	3,163	3,120
Bahi	2,885	3,171	3,127
Chamwino	2,873	3,159	3,115
Chemba	2,904	3,190	3,146
Kondoa	2,911	3,196	3,153
Kongwa	2,875	3,161	3,117
Mpwapwa	2,879	3,164	3,121
Mpwapwa (Chipogoro)	2,891	3,176	3,133
Mtera (Makatopora)	2,897	3,182	3,139
Mvumi	2,884	3,170	3,127
Geita	2,985	3,270	3,227
Bukombe	2,974	3,259	3,216
Chato	3,006	3,291	3,248
Mbogwe	3,023	3,308	3,265
Nyang'hwale	3,000	3,285	3,242
Iringa	2,883	3,169	3,125
Ismani	2,889	3,174	3,131
Kilolo	2,888	3,173	3,130
Mufindi (Mafinga)	2,893	3,179	3,135
Mufindi (Igowole)	2,902	3,187	3,144
Kagera (Bukoba)	3,035	3,320	3,277
Biharamulo	3,009	3,294	3,251
Karagwe (Kayanga)	3,051	3,337	3,293
Kyerwa (Ruberwa)	3,057	3,342	3,299
Muleba	3,035	3,320	3,277
Ngara	3,023	3,308	3,265
Misenyi	3,043	3,329	3,285
Katavi (Mpanda)	2,977	3,262	3,219
Mlele (Inyonga)	2,959	3,244	3,201
Mpimbwe (Majimoto)	2,996	3,281	3,238
Tanganyika (Ikola)	2,995	3,280	3,237
Kigoma	2,982	3,267	3,224
Uvinza (Lugufu)	2,972	3,257	3,214
Muyobozi Village (Uvinza)	2,980	3,265	3,222
Ilagala Village (Uvinza)	2,982	3,268	3,224
Buhigwe	2,980	3,265	3,222
Kakonko	2,982	3,268	3,224
Kasulu	2,991	3,276	3,233
Kibondo	2,988	3,274	3,230

JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Kilimanjaro (Moshi)	3,026	3,387	3,135
Hai (Bomang'ombe)	3,029	3,390	3,138
Mwanga	3,019	3,380	3,128
Rombo (Mkuu)	3,042	3,403	3,156
Same	3,012	3,373	3,121
Siha (Sanya Juu)	3,032	3,393	3,142
Lindi	2,889	3,257	3,120
Lindi-Mtama	2,894	3,262	3,138
Kilwa Masoko	2,913	3,281	3,095
Liwale	2,925	3,293	3,141
Nachingwea	2,909	3,277	3,149
Ruangwa	2,915	3,283	3,151
Manyara (Babati)	3,070	3,431	3,184
Hanang (Katesh)	3,081	3,442	3,194
Kiteto (Kibaya)	3,085	3,446	3,195
Mbulu	3,083	3,444	3,196
Simanjiro (Orkasumet)	3,102	3,463	3,216
Mara (Musoma)	2,985	3,270	3,227
Musoma Vijijini (Busekela)	2,998	3,283	3,240
Rorya (Ingirijuu)	2,992	3,277	3,234
Rorya (Shirati)	3,000	3,285	3,242
Bunda	2,976	3,262	3,218
Bunda (Kisorya)	2,989	3,274	3,231
Butiama	2,982	3,268	3,224
Serengeti (Mugumu)	2,993	3,279	3,235
Tarime	2,994	3,279	3,236
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,999	3,285	3,241
Mbeya	2,926	3,212	3,168
Chunya	2,936	3,221	3,178
Chunya (Makongolosi)	2,941	3,227	3,183
Chunya (Lupa Tingatinga)	2,943	3,228	3,185
Kyela	2,942	3,227	3,184
Mbarali (Rujewa)	2,910	3,196	3,152
Rujewa (Madibira)	2,924	3,209	3,166
Rujewa (Kapunga)	2,920	3,206	3,162
Rungwe (Tukuyu)	2,935	3,221	3,177
Morogoro	2,844	3,130	3,086
Mikumi	2,860	3,145	3,102
Kilombero (Ifakara)	2,882	3,167	3,124
Kilombero (Mlimba)	2,904	3,190	3,146

JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Kilombero (Mngeta)	2,894	3,179	3,136
Ulanga (Mahenge)	2,893	3,178	3,135
Malinyi	2,903	3,188	3,145
Kilosa	2,863	3,148	3,105
Gairo	2,863	3,148	3,105
Mvomero (Wami Sokoine)	2,855	3,140	3,097
Mvomero (Sanga Sanga)	2,844	3,130	3,086
Turian	2,869	3,155	3,111
Mtwara	2,875	3,244	3,134
Nanyumbu (Mangaka)	2,912	3,280	3,183
Masasi	2,891	3,260	3,159
Newala	2,896	3,264	3,166
Tandahimba	2,889	3,257	3,159
Nanyamba	2,889	3,257	3,159
Mwanza	2,969	3,255	3,211
Kwimba	2,987	3,273	3,229
Magu	2,977	3,263	3,219
Misungwi	2,964	3,249	3,206
Sengerema	3,002	3,287	3,244
Ukerewe	3,029	3,314	3,271
Njombe	2,912	3,197	3,154
Njombe (Kidegembye)	2,932	3,218	3,174
Ludewa	2,950	3,235	3,192
Makambako	2,904	3,189	3,146
Makete	2,943	3,228	3,185
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,909	3,195	3,151
Rukwa (Sumbawanga)	2,992	3,278	3,234
Sumbawanga Rural (Mtownisa)	2,992	3,278	3,234
Kalambo (Matai)	2,999	3,285	3,241
Nkasi (Namanyelete)	3,006	3,291	3,248
Nkasi (Kirando)	3,015	3,301	3,257
Ruvuma (Songea)	2,961	3,329	3,185
Mbinga	2,973	3,342	3,197
Namtumbo	2,952	3,320	3,190
Nyasa (Mbamba Bay)	2,999	3,367	3,207
Tunduru	2,926	3,294	3,164
Shinyanga	2,948	3,233	3,190
Kahama	2,953	3,238	3,195
Kishapu	2,956	3,241	3,198
Ushetu (Nyamilangano)	2,964	3,250	3,206

JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

Mji	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Ushetu (Kangeme Village)	2,970	3,255	3,212
Salawe	2,962	3,247	3,204
Simiyu (Bariadi)	2,966	3,251	3,208
Busega (Nyashimo)	2,978	3,263	3,220
Itilima (Lagangabilili)	2,966	3,251	3,208
Maswa	2,960	3,245	3,202
Meatu (Mwanhuzi)	2,971	3,256	3,213
Singida	2,910	3,195	3,152
Iramba	2,922	3,207	3,164
Manyoni	2,895	3,180	3,137
Itigi (Mitundu)	2,910	3,195	3,152
Ikungi	2,905	3,191	3,147
Mkalama (Nduguti)	2,934	3,220	3,177
Songwe (Vwawa)	2,936	3,221	3,178
Songwe (Mkwajuni)	2,942	3,228	3,185
Ileje	2,939	3,225	3,182
Momba (Chitete)	2,945	3,230	3,187
Tunduma	2,940	3,225	3,182
Tabora	2,927	3,213	3,169
Igunga	2,927	3,213	3,169
Kaliua	2,940	3,226	3,183
Ulyankulu	2,938	3,223	3,180
Nzega	2,938	3,223	3,180
Sikonge	2,936	3,222	3,178
Urambo	2,937	3,223	3,179
Uyui	2,934	3,219	3,176
Mpyagula	2,959	3,244	3,201
Tanga	2,979	3,340	3,107
Handeni	3,000	3,361	3,087
Kilindi	3,015	3,376	3,121
Korogwe	2,992	3,353	3,100
Lushoto	3,001	3,362	3,110
Mkinga (Maramba)	2,986	3,347	3,122
Muheza	2,984	3,345	3,107
Pangani	2,986	3,347	3,114

JEDWALI 2: BEI KIKOMO ZA JUMLA KWA SHILINGI/LITA

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	2,688.38	2,972.53	2,929.97
Tanga	2,848.16	3,207.70	-
Mtwara	2,744.10	3,111.10	-

Mha. Modestus M. Lumato
MKURUGENZI MKUU- EWURA